Ratiba ya Mafunzo Nyumbani kwa Chekechea

| Yaliyomo | Maoni ya Muda |
|---|---|
| **Soma vitabu, tazama vitabu zikisomwa kwa sauti ya juu** | **Dakika 20** |
| **Kompyuta au Teknolojia (Iliyoanzishwa darasani au mada katika eneo zilizoorodheshwa hapa chini)** | **Dakika 20** |
| **Hesabu** | **Dakika 20** |
| **Shughuli ya Kimwili** | **Dakika 20** |
| **Mchezo wa Herufi, Nyimbo, au Ufahamu wa Fonetiki** | **Dakika 20** |
| **Sayansi, Elimu ya Kijamii, au Elimu ya Kijamii na Kihisia** | **Dakika 20** |
| **Shughuli za Kiwiliwili za Uratibu (kubadilisha, uchoraji, kuandika)** | **Dakika 20** |
| **Sanaa za Ubunifu (sanaa, muziki, dansi, yoga)** | **Dakika 20** |

**Kila wiki, Mpango wa Mafunzo ya Mbali kwa shule za Chekechea utakuwa na saa moja ya shughuli iliyopangiliwa** ikiwa na shughuli tatu au nne ndani ya mada zilizoorodheshwa hapa juu. Idara ya Utoto wa Mapema imepanga ratiba ya picha kwa Ukurasa wa Tovuti wa Chekechea ili kuwapatia wazazi wa wanafunzi wa chekechea chaguo za ratiba ya siku nzima ikiwa na utaratibu wa nyumba.

**Mafunzo ya Mbali:**

➢Mwalimu wa mtoto wako atawasiliana nawe ili kupanga wakati wa kufuatilia wanafunzi na kujadiliana kuhusu chaguo za kusaidia mwanafuzi kwa mafunzo ya mbali . Baadhi ya chaguo hizo zinaweza kuwa barua pepe, kuwasiliana kutumia Google Classroom, DOJO, Remind, au jukwaa zinginezo, au kuwa na vipindi vya kufuatilia wanafunzi kutumia Zoom au Google Hangouts. Mbinu hizi zitabadilika kulingana na darasa, na shule. Shule yako itawasiliana na familia moja kwa moja ili kutoa habari hii.

**Kazi za Nyumbani za Kila Wiki:**

➢Kila wiki wanafunzi watapokea shughuli ili kuboresha mafunzo ya mbali. Shughuli hizi zitabadilika kulingana na mada na zitatoa chaguo zaidi kwa wanafunzi na familia zao ili kuboresha kujifunza nyumbani.

Wanafunzi wetu wachanga zaidi watanufaika kutoka Kusoma kwa Sauti ya Juu wa vitabu na wazazi au ndugu zao wakubwa. Pia, unaweza kutembelea tovuti ya Shule ya Lowell Public School: Kusoma kwa Sauti ya Juu wa vitabu Shule ya the Cardinal O'Connell School ina hadithi nyingi zinazofaa watoto wadogo zinazowekwa kwa tovuti hilo. Unaweza kupata orodha ya vitabu za Kusoma kwa Sauti ya Juu zilizoandaliwa na Walimu wa Lowell Public School kupitia https://www.lowell.k12.ma.us/Page/3777

Tunawatia mafamilia moyo kurejelea *Mipango ya Kujifunza Nyumbani wa Chekechea* na kuchagua shughuli zinazosaidia kujifunza wa mapema katika mada za shule. Familia hazihitajiki kuwasilisha kazi kwa walimu kwa minajili ya chekechea, lakini walimu wetu wangependa kusikia kutoka familia kuhusu ushiriki wa wanafunzi kwa mashughuli kupitia barua pepe, picha au jukwa zingine.

Kwa wanafunzi wanaopokea huduma za elimu maalum, shughuli zitabadilishwa zinavyofaa kutumia ushirikiano kati ya mwalimu wa darasa na mwalimu wa elimu maalum. Unaweza kufikiria kuchunguza fursa za kujifunza kwenye mtandao zilizopendekezwa na mwalimu wa mtoto wako, inayopatikana katika *Mpango wa Kujifunza Nyumbani wa Chekechea* au itakayowekwa kwenye tovuti la LPS. Kazi hizi za nyumbani ni za hiari.

➢**Mikutano ya Mtandao na Wanafunzi –** Mwalimu wa mtoto wako atawasiliana nawe kuhusu maelezo na wakati wa mikutano haya ya mtandao. Kushiriki katika mikutano haya ni hiari kwa watoto na familia. Kwa wanafunzi wanaopokea huduma za elimu maalum ya kutolewa kwa darasa la kawaida, watoa huduma wa elimu maalum watakuwa na muda tofauti ili kuwasiliana na wafunzi ambao wanapokea huduma, inavyofaa.

Tunawatia moyo familia kuandaa ratiba zao wenyewe unaolingana na hali yao ya kipekee. Tunakutia moyo ujishirikishe na masomo ya mbali inayokufaa na shughuli zinazoambatana. Fursa ya mkutano wa mtandao unaweza kupatia mtoto wako fursa ya kuonana na rafiki wake kutoka shule wanaposhiriki katika shughuli pamoja na mwalimu wake. Panga ratiba ya wiki hiyo inayolingana na familia yako and supports your child's learning. Watoto wengi hufanikiwa wanapotumia taratibu na matarajiyo yanayoweza kutabirika. Unaweza kutumia ratiba ya picha iliyo hapa chini ili kukusaidia wewe na mtoto wako kuanzisha utaratibu unaokidhi hitaji la familia iwapo watoto hawako shuleni.

Ratiba ya Mafunzo Nyumbani kwa Chekechea

## Ratiba ya Picha ya Kila Siku

**Ratiba na hali ya familia ya kila mtu ni tofauti, kwa hivyo unaweza kuweka nyakati zinazokufaa wewe zaidi. Pamoja na uangalifu unayotekelezwa na wazazi (dakika kumi na tano) na usaidizi wa kuanzisha, watoto wanaweza kuwa huru**

**Mnamo wakati wa mradi, kucheza ndani ya nyumba, na wakati wa kimya. Chagua mashughuli yatakayo kufurahisha wewe na/au mtoto wako.**

| **Wakati** | Shughuli |
|---|---|
| **Asubuhi** |  **Kiamsha Kinywa** |
| **Asubuhi** |  **Piga Mswaki**  **Saidia katika Usafi** |
| **Asubuhi** | **Wakati wa Hadithi**  **chora na andika**  |
| **Asubuhi** | **Enda Nje**   |
| **Asubuhi** | **Wakati wa Mradi – Safisha Unapomaliza**   |

| | |
|---|---|
| **Alasiri** | **Chakula cha Mchana na usaidizi ndani ya nyumba**<br>  |
| **Alasiri** | **Wakati wa Kimya na Kucheza nje ya nyumba**<br>   |
| **Alasiri** | **Kucheza na Kujifunza – Safisha Unapomaliza**<br>  |
| **Alasiri** | **Nyimbo na dansi**<br> |
| **Alasiri** | **Safisha ala za mchezo na saidia katika shughuli za nyumba**<br>  |

# Muhtasari wa Elimu ya Mbali kwa Familia za Chekechea

| | |
|---|---|
| Jioni | Chajio  |
| Jioni | Wakati wa familia   |
| Jioni | Hadithi ya usiku  Usiku mwema  |

# Muhtasari wa Elimu ya Mbali kwa Familia za Chekechea

https://www.somervilleearlyed.com/schoolhomecurriculum